# Kiswahili na Sera ya Elimu katika Shule za Sekondari Nchini Kenya

*Dunstan Kwova Egessa*[1] *na Isaac Ipara Odeo*[2]
[1]*Chuo cha Ualimu cha Migori*
[2]*Chuo Kikuu cha Kibabii*

**Ikisiri**

**Makala haya yanachunguza matatizo yanayowakumba walimu katika utekelezaji wa silabasi ya sasa ya Kiswahili. Utafiti ulifanywa katika Kaunti ya Kakamega, Mkoa wa Magharibi nchini Kenya. Sampuli ya watafitiwa iliteuliwa kwa kutumia mbinu za utabakishaji, uwiano na njia nasibu sahili. Walimu 70 na walimu wakuu 43 walishiriki katika utafiti. Afisa wa Usanifu wa Viwango vya Elimu mmoja na Mkuza mitalaa mmoja katika Taasisi ya Elimu Kenya walishiriki kama watafitiwa maalumu. Nyenzo za ukusanyaji data ambazo zilitumiwa ni hojaji, mwongozo wa masaili na mwongozo wa uchunzaji. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Uwezeshaji ya Carl Rodgers. Utafiti uligundua kwamba utekelezaji wa silabasi ya sasa ya Kiswahili unakumbwa na matatizo mbalimbali. Sababu za hali hii ni kuwa, walimu hawakuandaliwa mapema kabla ya kuanzishwa kwa silabasi hii na wengi katika vyuo hawakujifunza baadhi ya mada katika silabasi ya sasa ya Kiswahili. Walimu, vile vile, hawaandaliwi mafunzo nyanjani na walimu hawajiandai vyema kitaaluma. Ili walimu waweze kufaulisha utekelezaji wa silabasi, utafiti umependekeza kuwa, Taasisi ya Elimu ya Kenya iandae semina kadhaa kwa walimu Kauntini ili masuala nyeti katika silabasi yafafanuliwe. Wizara ya Elimu yafaa itenge fedha za kufadhili mafunzo kwa walimu kwa Kiswahili nyanjani pamoja na usimamizi. Aidha, vyuo vinavyoandaa walimu wa shule za upili vitilie maanani mada ambazo zinajumuishwa katika mitalaa ya shule za upili. Mwisho walimu wazingatie maadili ya kazi yao.**

**Maneno Muhimu:** *Sera ya elimu, Kiswahili, Utekelezaji, Kenya*

## Utangulizi

Mabadiliko ya mifumo ya elimu ni jambo la kawaida katika nchi yoyote ile. Mabadiliko hutokea kutegemea mpito wa wakati na mahitaji ya nchi. Kadiri mifumo ya elimu inavyobadilika, ndivyo mitaala hubadilika. Mabadiliko huweza kutokea katika mtaala mzima au somo maalumu. Kutekelezwa kwa mageuzi haya huhitaji kuwekwa kwa sera. Sera, kwa maana inayotolewa na Kamusi ya Kiswahili

Sanifu (2004) ni utaratibu wa kuendesha jambo ili kukidhi haja za serikali (au asasi yoyote ile).

Sera katika masuala ya kielimu hutoa matamko kuhusu idadi ya vipindi, maudhui ya kufundishwa, njia na nyenzo za kufundishia, mbinu za kutathmini, maandalizi ya walimu na kadhalika. Tangu 1985, silabasi ya Kiswahili sekondari katika mfumo wa elimu wa 8-4-4 ilipoundwa na kuanza kutumiwa, imepitiwa mara tatu; mapitio yalifanywa kwanza mwaka 1992 halafu ya pili mwaka 1997. Lakini mapitio hayo yalikuwa madogo.

Mapitio ya mara ya tatu ya silabasi ya Kiswahili ya shule za sekondari iliyozinduliwa 1985 na yaliyofanywa mwaka 2002 ndiyo yalikuwa makubwa zaidi. Haya yalifanywa kwa lengo la kusawazisha maudhui. Kwa mara ya kwanza katika historia ya somo la Kiswahili, utaratibu uliwekwa ili kuingiza kwenye silabasi maudhui mapya, kuondoa maudhui mengine, kubadilisha namna ya kushughulikia baadhi ya maudhui na kusisitiza ukati wa njia shirikishi na nyenzo za kufundishia. Hali kadhalika, Taasisi ya Elimu nchini Kenya (ambayo imebadilishwa jina na kuitwa Taasisi ya Ukuzaji Mitaala) imeweka sera kuhusu idadi ya vitabu vya kiada na vya ziada (Kenya Institute of Education, 2002; 2006). Kuzinduliwa kwa silabasi hii mwaka 2003 kumezua hisia tofautitofauti baina ya wazazi, walimu, wanafunzi na wachapishaji. Baadhi yao wameishangilia silabasi mpya lakini wengine wamelalamika. Hivyo basi, imekuwa muhimu kuhakiki utekelezaji wake. Katika makala haya, tumezingatia matokeo ya utafiti uliojifunga kwenye nafasi ya walimu. Uamuzi huu umetokana na sababu kwamba walimu ndio wenye nafasi ya kikati katika utekelezaji wa sera za mitaala shuleni (Bishop, 1995; Asiachi, 1986). Kwa jinsi hii, mtazamo wao na utendaji kazi wao unaweza kuathiri utekelezaji na hatimaye ufanisi wa mitaala. Hivyo basi, ni muhimu kutafitia namna walimu wanaandaliwa au wanavyojiandaa ili wakabiliane na jukumu la kutekeleza silabasi.

Utafiti ulifanywa katika kaunti ya Kakamega, Mkoa wa Magharibi nchini Kenya. Eneo hili liliteuliwa kwa sababu lina shule nyingi za vijijini ambazo zinaakisi hali ya shule nyingi za sekondari nchini. Ni katika shule kama hizi ndipo walimu hukumbwa na changamoto nyingi za kutekeleza mitaala. Mtagusano kati ya watafiti na walimu ulionyesha kuwa idadi kubwa ya walimu katika kaunti hii wanatingwa na ndaro kadha wa kadha katika juhudi zao za kufanikisha utekelezaji wa silabasi ya Kiswahili (KIE, 2002). Watafiti walitumia njia tatu za kuteua sampuli:- utabakishaji, uwiano na nasibu. Kaunti ya Kakamega ilikuwa na jumla ya walimu 235 wanaofunza Kiswahili katika shule mbalimbali kwa mujibu wa kumbukumbu za Mei 2005 katika afisi ya Mkuu wa Elimu Kaunti ya Kakamega. Walimu 70 waliteuliwa kuunda sampuli ya utafiti. Hii ni asilimia thelathini ya walimu wa Kiswahili kauntini.

Katika ukusanyaji data, utafiti ulitumia hojaji, masaili, uchunzaji na uchanganuzi wa nyaraka. Matumizi ya nyenzo anuwai uliweza kuimarisha uaminifu na kuthibitisha data. Picciana (2004) anaeleza kwamba matumizi ya nyenzo zaidi ya moja huziwezesha kujalizana na hivyo kuhakikisha ukamilifu na ubora wa data

inayokusanywa. Uchanganuzi wa data ulifanywa kwa njia za kitarakimu na kiuhakiki. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uwezeshaji. Waasisi wa nadharia hii ni Carl Rodgers na wenzake (Laird, 1985). Nadharia ya uwezeshaji inamlenga mwalimu moja kwa moja kama mtekelezaji wa masuala ya kielimu. Mhimili wa nadharia hii ni kuwa ufanisi wa mafunzo utawezekana tu iwapo mwalimu ataanda(liw)a mazingira shwari ambamo mwanafunzi atahisi utulivu na kupokea dhana mpya bila usumbufu. Kwa hivyo, watafiti walionelea kuwa mwalimu anayefaa kwa jambo hili ni lazima awe ni yule aliyepata maandalizi bora.

**Matokeo ya Utafiti**

Utafiti huu ulidhihirisha hali halisi inayohusiana na mwalimu wa Kiswahili na ambayo inamfanya asiweze kutekeleza silabasi mpya ya Kiswahili kikamilifu kulingana na matarajio. Matokeo yatakayowasilishwa na kujadiliwa hapa chini yanammulika mwalimu akiwa chuoni na nyanjani. Utafiti uligundua kwamba walimu wote ambao walitafitiwa walikuwa wamefuzu kutoka vyuo tofauti tofauti katika viwango mbalimbali vya kitaaluma. Asilimia 77 walikuwa na shahada ya kwanza, 19% walikuwa na stashahada na 4% walikuwa na shahada ya uzamili. Kila moja ya walimu hawa alikuwa amefuzu kufunza Kiswahili pamoja na somo moja lingine zaidi. Aidha, uchanganuzi wa data ulifichua kuwa ingawa walimu hawa walifuzu kufundisha Kiswahili, utendaji wa 70% ya walimu ulionyesha kuwa hawakukamilika katika maandalizi yao ya vyuoni. Ilitokea kwamba asilimia 36 ya walimu hawa hawakuwa wamejifunza kozi ambazo maudhui yake yametiliwa mkazo katika silabasi ya sasa ambayo walitakiwa kutumia kufundisha katika shule za upili. Maudhui haya ni kama vile isimujamii, fasihi simulizi, hadithi fupi na uchanganuzi wa sentensi (KIE, 2002).

Mahojiano na baadhi ya walimu waliojumuishwa kwenye sampuli yalifichua kuwa hawakujiamini walipohitajika kufunza mada ambazo hawakuzipitia vyuoni. Jambo hili liliwapelekea walimu wengine kutaka mada hizi zichunguzwe upya. Changamoto inayowakumba walimu wa Kiswahili inatinga utekelezaji wao wa silabasi ya Kiswahili katika shule za upili. Uchunguzi ulibainisha kuwa hali hii imesababishwa na utaratibu unaofuatwa na vyuo vikuu katika maandalizi ya walimu wa Kiswahili ambao hauzingatii mitaala ya shule za sekondari.

Nyaraka za baadhi ya vyuo vikuu kama vile WUCST (2004) na Chuo Kikuu cha Nairobi (2004/5) zilipochunguzwa, tofauti katika kutayarisha walimu wa Kiswahili ilijitokeza. Ilidhihirika kuwa kozi fulani zinaweza kuwa za lazima katika chuo kimoja na sio katika chuo kingine. Jambo hili huwapa wakurufunzi nafasi ya kudondosha masomo mengine hata ikiwa yanahitajika katika silabasi ya shule za upili. Baada ya kufuzu, walimu huhisi wana upungufu na wakikabiliana na mada ambazo hawakuzishughulikia katika vyuo vikuu.

Ilibainika kuwa vyuo vikuu havina utaratibu unaolingana. Linalotendeka ni kuwa, vyuo tofauti huweza kufunza kozi tofauti tofauti. Tatizo ni kuwa hao walimu ambao wamefunzwa kutoka vyuo tofauti wanaishia kufunza shule ambazo zina

mtalaa sawa. Hata hivyo, tofauti kwa misingi ya vyuo vikuu walivyosomea ualimu hazikubainika katika utafiti. Kuna haja ya utafiti zaidi kuhusu suala hili. Jambo lingine ambalo linawazonga walimu katika utekelezaji kikamilifu wa silabasi ya Kiswahili ni sera ya walimu kufunza masomo mawili katika shule za upili. Katika vyuo vikuu, walimu huandaliwa kufundisha Kiswahili na somo lingine zaidi kama historia jiografia na kadhalika. Hii inatokana na sera ya Tume ya Kuwajiri Walimu ambapo mwalimu aliyefuzu anahitajika kufunza Kiswahili na somo lingine.

Suala la walimu wa Kiswahili kufunza masomo mengine linaelekea kuleta shaka kidogo kwa wanaojali umilisi wa lugha wa wahitimu wa shule za sekondari kwani wanashughulikia mambo mengi kwa wakati mmoja. Hali ya kuandaa mwalimu kufunza masomo mengi humnyima fursa ya kuzamia somo moja kikamilifu. Chi, na wenzake (1988) wanasema kuwa weledi huimarika ambapo mhusika hubobea sana uwanja mmoja na siyo nyanja kadhaa. Kwa hivyo, walimu wa Kiswahili wanaweza kufunza vyema iwapo hawatajifunza wala hawatafunza masomo mengine. Utaratibu wa vyuo vikuu huwapa wakurufunzi wa somo la Kiingereza fursa ya kufuzu katika somo hili pekee. Hata baadhi ya walimu wa somo la hisabati huruhusiwa kusomea somo hilo tu na huweza kufuzu. Mpango huu huwapa walimu wa Kiingereza au hisabati nafasi ya kupitia mambo mengi katika somo husika kuliko wale walimu wa Kiswahili ambao wana masomo mengine.

Jambo lingine ambalo lilifichuka katika utafiti wetu na linalowatatiza walimu ni kutoelewa mabadiliko yaliyowekwa katika silabasi ya sasa. Jamii ni asasi ambayo haibaki tuli. Mahitaji ya jamii hubadilikabadilika kila uchao. Kwa sababu hii, mitalaa ya elimu lazima ichunguzwe upya ili iweze kuakisi mahitaji haya kwa manufaa ya nchi na wazalendo wake. Bishop (1995) anashauri kuwa ili mabadiliko katika elimu yawe na ufanisi, ni lazima yafanywe kiurazini na kwa kusudi fulani. Bila urazini, kuna uwezekano wa kuwa na mfumo ambao hauambatani na matakwa ya taifa. Tathmini ya kitaifa iliyofanywa na Taasisi ya Elimu ya Kenya mwaka 1999 kwa jina "the National Assessment Survey" (KIE, 1999) ndiyo ilikuwa msingi wa kubadilisha silabasi ya Kiswahili ya shule za upili.

Utafiti uliofanywa na waandishi wa makala haya ulilenga kujua iwapo walimu walifahamu mabadiliko kuhusu vipengee vya malengo, mada, njia za kufunzia, nyenzo za kufundishia na tathmini ya jinsi mambo haya yanavyojitokeza katika silabasi. Kati ya walimu 70 walioshiriki katika utafiti, takwimu zinaonyesha kuwa 76% ya walimu wana ufahamu mzuri wa malengo ya silabasi, ilhali 64% wanafahamu mada na 69% wanajua njia za kufundishia. Halikadhalika, utafiti uligundua kuwa nyenzo za kufundishia hazikufahamika vyema kwa 63% ya walimu. Mbinu za kutathmini katika silabasi mpya hazikufahamika kwa 71% ya walimu kufikia wakati data ilipokusanywa.

Takwimu hizi zinaonyesha kuwa katika shule kuna idadi kubwa ya walimu ambao hawajafahamu mabadiliko katika silabasi ya sasa. Ikiwa mwalimu haelewi malengo na mada katika somo la Kiswahili, basi ni wazi kwamba hawezi hata kufikiri juu ya njia za kufunzia na namna ya kutathmini mambo haya. Gross na

wenzake (1971) wanasema kuwa hali ya walimu kukosa uwezo wa kuafiki wajibu wao mpya ni kizuizi kikubwa katika utekelezaji wa mtalaa mpya. Silabasi ya Kiswahili ilianza kutumika shuleni mwaka wa 2003. Utafiti ulifichua kuwa Baraza la Mitihani halikutuma barua ya taarifa (KNEC/SDS/CS/KCSE/05/003) kuhusu muundo mpya wa mtihani kwa shule zote nchini hadi baada ya tarehe 22/03/05. Tangu 2003 hadi 2005 walimu hawakujua muundo wa tathmini. Uchunguzi wa nakala za tathmini zilizotungwa na walimu mbalimbali ulionyesha kwamba tathmini hizi zilitofautiana kimuundo kwa sababu walimu hawakuwa na mwongozo wa kuzingatia.

Kulingana na Farrant (2000), tathmini ya ufanisi wa ujifunzaji ni muhimu darasani kwa vile humwezesha mwalimu kufahamu uwezo na udhaifu wa wanafunzi. Vile vile, tathmini humzindua mwalimu kwa kumwezesha kupima utendaji wake mwenyewe. Ikiwa walimu hawakumudu kipengele cha msingi kama hiki, ni wazi kuwa utekelezaji wa silabasi utakumbwa na matatizo. Walimu walihitajika kuonyesha ikiwa wamewahi kuhudhuria semina au warsha yoyote kati ya mwaka 2000 na 2005. Matokeo ya utafiti kuhusu mahudhurio ya semina yalidhihirisha hali isiyoridhisha. Zaidi ya 50% ya walimu waliotafitiwa walikiri kuwa hawajawahi kushiriki katika semina ya aina yoyote. Katika kipindi hicho, walimu chini ya 50% walidai wamehudhuria angalao semina tatu.

Uchanganuzi wa barua za mwaliko ulifichua kwamba semina hizo ziliandaliwa na mashirika ya kibinafsi. Jambo lililoshughulikiwa katika semina lilikuwa ni uchambuzi wa vitabu vya fasihi vilivyopendekezwa kwa minajili ya mitihani ya kitaifa ya kidato cha nne. Majadiliano kati ya watafiti na walimu yalidokeza kwamba hali hii ya ufinyu wa mada katika semina hizi haikuwafurahisha walimu. Walimu walitaka vipengele zaidi vya ufundishaji wa lugha viwasilishwe. Semina humwezesha mwalimu kufahamu mabadiliko yanayotokea mara kwa mara katika mtalaa na somo analofundisha (Stima, 1988; Shiundu & Omulando, 1992). Kwa mfano, semina inaweza kulenga mada mpya katika silabasi, njia za kufundishia, matumizi ya aina fulani ya vitabu vya kiada na kadhalika. Ni dhahiri kwamba mwalimu asiye na umilisi katika jambo fulani anaweza kuimarika ikiwa atahudhuria semina.

Kutokana na utafiti, iligunduliwa kuwa hapakuweko na semina ambayo ilitayarishwa kwa ajili ya walimu na Wizara ya Elimu au Taasisi ya Elimu ya Kenya kati ya mwaka 2000 na 2005. Taasisi ya Elimu ya Kenya ni asasi ambayo imepewa jukumu kubwa la kukuza mitalaa ya elimu nchini Kenya. Kati ya shughuli zake mahsusi ni kuandaa semina za kuwatanabahisha walimu juu ya mabadiliko katika silabasi. Kwa sababu hii, inaweza kuchukuliwa kwamba walimu hawakushirikishwa au kuandaliwa na Taasisi ya Elimu ya Kenya ili wawe katika nafasi nzuri ya kukabiliana na silabasi inayotumika katika kiwango cha shule za upili.

Bishop (1995), Hawes (1999), na Urevbu (1999) wanashikilia kuwa mwalimu lazima ashirikishwe katika ukuzaji wa mitalaa. Kwao, mwalimu ana nafasi ya ukati kwani ndiye mtekelezaji mkuu wa mtalaa. Vilevile, watafiti walishughulika na

uchunguzi wa utendaji wa Idara ya Usanifu wa Viwango vya Elimu. Idara hii ni kiungo muhimu kati ya walimu, Wizara ya Elimu na Taasisi ya Elimu ya Kenya. Idara hii husimamia utekelezaji wa mtalaa nyanjani.

Jambo lililobainika kutokana na uchanganuzi wa data ni kuwa utendaji wa maafisa wa usanifu wa viwango vya elimu ni hafifu. Maafisa hawa hawatembelei shule mara kwa mara ili kuwashauri walimu kuhusu kazi yao. Walimu wakuu walifichua kuwa "shule ndogo" hazithaminiwi na maafisa wa elimu kauntini na kutembelewa kwao ni haba mno. Hata mwaka mzima unaweza kupita bila afisa yeyote kuzuru shule hizi. Afisa mmoja wa usanifu wa viwango vya elimu aliyehojiwa alitoa sababu mbili kama kizuizi kwa kazi yao. Kwanza, idadi ya maafisa ambao wanashughulikia shule za upili kaunti ya Kakamega ni ndogo sana. Kuna maafisa wanane kwa shule 109. Kati ya hawa wanane, afisa anayehusika na Kiswahili ni mmoja tu. Pili, kulikuwa na upungufu wa pesa ambao uliwalemaza kila walipotaka usafiri wa kwenda shuleni na vile vile kuandaa semina mbalimbali kwa walimu.

Kwa mujibu wa African Curriculum Organization (ACO, 1979), kuingiliana kwa maafisa wa elimu na walimu ni kwa manufaa ya walimu na wadau wengine katika nyanja ya elimu. Walimu, kupitia kwa maafisa hawa, huweza kupata mwongozo bora kuhusu utendaji wao kazini. Vile vile, walimu huweza kujulishwa juu ya mabadiliko mapya katika masomo wanayofunza na matarajio ya Wizara ya Elimu kuhusu ufundishaji. Taasisi ya Elimu ya Kenya hutegemea maafisa hawa wa nyanjani kuleta mrejesho kuhusu utekelezaji wa silabasi shuleni. Jinsi hali ilivyo, Taasisi ya Elimu ya Kenya haipati mrejesho unaohitajika na, kwa hivyo, haipati tathmini mwafaka kuhusu utekelezaji wa silabasi.

Katika maandalizi yao ya kibinafsi kabla ya kwenda darasani, watafiti waligundua kuwa walimu wengi hupuuza mambo mengi ya kimsingi. Ilijitokeza katika uchunzaji kuwa walimu wengi hawakuwa na stakabadhi muhimu za kuegemea kama mwongozo wakati wa kufunza. Inashangaza kuwa walimu hawakuzingatia matumizi ya maazimio ya kazi, andalio la somo, kumbukumbu ya kazi, n.k. Isitoshe, wengi hawakujitahidi kutafuta nyenzo za kufundishia. Ukosefu wa stakabadhi hizi na nyenzo za kufundishia huweza humnyima mwalimu mantiki na muelekeo katika kutoa mafunzo darasani.

## Mapendekezo

Utafiti ulifichua kwamba iliyokuwa Taasisi ya Elimu ya Kenya wakati huo haikutayarisha walimu kabla ya kupeleka silabasi mpya shule. Ili kuondoa hali ya suitafahamu kwa walimu, Taasisi inaweza kuandaa semina kadhaa kwa walimu katika kaunti ili masuala nyeti kuhusu silabasi ya sasa yafafanuliwe. Kwa mfano, mada, njia za kufunzia na kutathmini na kadhalika. Masuala haya yakishaelezwa, walimu watakuwa katika nafasi nzuri ya kutimiza malengo ya silabasi hii. Vile vile, semina hizi zitakuwa uwanja mzuri wa Taasisi kupata mrejesho kuhusu silabasi kutoka kwa walimu wenyewe.

Hali nyingine ambayo inaweza kuimarisha utekelezaji wa silabasi ni Wizara ya Elimu kufadhili (au kutafuta ufadhili) walimu wanaohudumu waweze kuandaliwa semina, warsha na makongamano ya mara kwa mara. Makongamano haya yatawasaidia walimu kujipiga msasa kuhusiana na mapana na marefu ya Kiswahili. Ni muhimu makongamano haya yawahusishe walimu wenye tajriba mbalimbali; wahadhiri wa vyuo vikuu na wataalamu wengine ambao kuhusishwa kwao kutamjenga mwalimu wa Kiswahili kitaaluma na kiakademia.

Wizara ya Elimu, vile vile, inahitajika kuhakikisha ufadhili wa kutosha kwa shughuli za maafisa wa usanifu wa viwango vya elimu wanaohusika na masomo, likiwemo somo la Kiswahili. Mtagusano kati ya walimu na maafisa hawa unaweza kuimarisha hali ya ufundishaji wa Kiswahili iwapo utendaji kazi wao utaongozwa na maadili ya kikazi. Maafisa hawa wasiwe watu wa kuwatia hofu na kuwakashifu walimu bali wawe na jukumu la kushauri na kurekebisha makosa na kufumbua matatizo.

Pendekezo lingine ni kwa vyuo ambavyo vinawaandaa walimu wa Kiswahili wa shule za upili. Ni muhimu vyuo hivi viweke utaratibu ambao unahakikisha kwamba maudhui yaliyomo kwenye silabasi ya shule za sekondari yamejumuishwa katika kozi za wanafunzi wao. Aidha, kozi ambazo zinashughulikia mada hizi ziwe za lazima kwa kila mwanafunzi anayenuia kufundisha Kiswahili. Mpango huu utakomesha tatizo la walimu shuleni kushindwa kufunza mada fulani kwa kisingizio kuwa hawakujifunza vipengele hivyo katika vyuo na vyuo vikuu.

Utafiti huu unapendekeza kuwa walimu wa somo la Kiswahili katika shule za upili yapasa wazingatie maadili ya taaluma. Walimu wawe wenye bidii kazini, wafanye maandalizi yanayohitajika kuhusu: kutengeneza maazimio ya kazi, mpangilio wa somo, na kumbukumbu za kazi. Halikadhalika, walimu wanahitaji kuwa watafiti ili waweze kutambua mambo mengi ambayo hawayafahamu kuhusu (ma)somo wanayofundisha shuleni.

## Hitimisho

Makala haya yamejadili suala zima la utekelezaji wa silabasi ya sasa ya Kiswahili (KIE, 2002) katika shule za upili kaunti ya Kakamega hautimiziki ipasavyo. Walimu wa Kiswahili wanakumbwa na matatizo ya aina mbili: Kwanza ni yale ambayo yanasababishwa na asasi zinazohusiana na ukuzaji wa elimu ambazo ni Taasisi ya Elimu ya Kenya, Wizara ya Elimu na vyuo vikuu. Pili, walimu wana matatizo ya kibinafsi kama kutotilia maanani umuhimu wa kujiandaa vilivyo kabla ya kwenda darasani. Imebainishwa kuwa matatizo ya aina zote yanaweza kutatuliwa kwa juhudi za pamoja.

**Marejeleo**

ACO. (1979). Basic Training course inSystematic Development. Nairobi: KIE.

Asiachi, A. & Oketch, J. (1986). Curriculum Development in Primary Schools. Nairobi: Kenyatta University ODA series.

Bishop, G. (1995). Curriculum Development: A text book for students. Hong Kong: Macmillan Education Ltd.

Chi, M. T. H. na wengine (1988). The Nature of Expertise. New Jersey: Hillsdale.

Farrant, J. S. (2002). Principles and Practice of Education. Singapore: Longman Group U.K.

Gross, na wenzie (1971). Implementation of Organizational Innovation: A Sociological Analysis of Planned Change. New York: Basic Books Inc. Publishers.

Hawes, H. (1979). Curriculum Reality in African Primary Schools. London: Longman Group.

Kenya Institute of Education (1999). National Assessment Survey. Nairobi: KIE.

Kenya Institute of Education (2002). Secondary School Syllabus Vol.1. Nairobi: KIE.

Kenya Institute of Education (2006). Kiswahili sekondari:Mwongozo wa mwalimu. Nairobi. KIE.

Kenya National Examinations Council (2005). KNEC/SDS/CS/KCSE/05/003 KCSE Subjects and Examination Format. Nairobi.

Liard, D. (1985). Approaches to Training and Development. Addison Wesley Reading, Mass.

Picciano, A. G. (2004).Educational Research Primer. London: Continuum. Katika Shiundu, J.& Omulando, S. (1992) Curriculum Theory and Practices in Kenya. Nairobi: Oxford University Press.

Sitima, T. (1988). "Issues of implementation of 8-4-4 programme and inspection of schools" Report of Educational Administration Conference. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

University of Nairobi. (2004). Academic Calendar. Nairobi: University of Nairobi Press.

Urevbu, A. (1999). Curriculum Studies. Lagos: Longman Nigeria Ltd.